**Huu ni mkusanyiko wa insha zinazohitaka katika mtaala wa elimu nchini Kenya hasa kwa wanafunzi wanojiandaa kwa mtihani wa kitaifa wa KCSE. Insha hizi zinafaa kutumiwa na mwalimu katika kuwaelekeza wanafunzi wanapofanya kazi yao ya kudurusu na wakati mwingine wanaposoma vipindi vya uandishi katika somo la Kiswahili. Martin Otundo (PhD fellow-JKUAT Mombasa Campus) ni mwalimu na mwandishi kando na kuwa mtafiti katika maswala mbalimabli. Martin pia ni mhadhiri katika vyuo vikuu mbalimbali katika eneo la Pwani mwa Kenya. Ashawaituzwa na mashirika mbalimblai barani Africa kama mtafit chipukizi.**

**martinotundo@gmail.com +254721246744**

Martin Otunod Richard +254721246744

**INSHA**

**Aina**

# 1. TUNGO ZA KIUAMILIFU

Ambazo hutekeleza kazi maalum na huwa na muundo maalum.Hizi hutokea kama swali la kwanza kwenye shule za upili.

### A) INSHA ZA BARUA

### 1. BARUA YA KIRAFIKI

Inayoandikwa kwa ndugu, jamaa na marafiki.

**Muundo**

a. Anwani ya mwandishi -(wima au mshazari/mlazo. Jina lisiwekwe!)
b. Tarehe ya kuandikwa barua -(22 Julai, 2016)
c. Mtajo- (Kwa … mpendwa/kwenu…
d. utangulizi (salamu, kumjuliana hali)
e. mwili/yaliyomo (ujumbe)
f. Hitimisho (Wasalimie jamaa wote/nawatakia mema/sinabudi kukomea papo
g. Thibitisho-Ni mimi wako/wenu, Jina (wima au mshazari)

### 2. BARUA RASMI

Inayoandikwa kwa shuguli rasmi/watu mahususi.

**Muundo**

i. Anwani ya mwandishi -(wima au mshazari/mlazo. Jina lisiwekwe!)
ii. Anwani ya mwandikiwa
iii. Tarehe ya kuandikwa barua -(23 Julai, 2016)
iv. Mtajo- (Kwa … BW/BI/PROF…
v. MINT/KUH/YAH: mada ya unachoandika barua kuhusu
vi. utangulizi (salamu, kumjuliana hali)
vii. mwili/yaliyomo (ujumbe)
viii. Hitimisho (Wasalimie jamaa wote/nawatakia mema/sinabudi kukomea papo
ix. Thibitisho-Ni mimi wako/wenu, Jina (wima au mshazari)

### 3. BARUA KWA MHARIRI

- Barua ambazo huandikwa na kutumwa ofisini kwa kutaka kuomba kazi, kuomba msaada, malalamiko, kutoa maoni gazetini, n.k.

**Muundo**

i. Anwani ya mwandishi (wima au mshazari)

ii. Tarehe ya kuandikwa (usiweke jina).
iii. Marejeleo - REJ: SUD/MSS/054/009 (nambari ya kumbukumbu, faili au nambari ya barua)
iv. Anwani ya mwandikiwa na cheo k.m. Mhariri wa Gazeti la 'Nation', S.L.P 89000, Nairobi.

**Iwapo ni mwanafunzi anaandika**

v. Kupitia kwa: MWALIMU MKUU, anwani
vi. Mtajo k.m. Kwa Bwana/Bibi/Profesa/Daktari/Mhubiri
vii. Kichwa cha barua k.m. MINT: KUENEZWA CHUKI KUPITIA GAZETI LAKO.
viii. Utangulizi

*(Mintaarafu ya chuki mliyoeneza kuhusu wakaazi wa matopeni nimeamua kusimama nao tisti kama kigongo na kukataa katakata jambo hilo. Kwa kweli insikitisha kuona gazeti imara kama hili likifanya haya…)*

ix. Mwili (matatizo, madhara, mapendekezo, shukrani n,k)
x. Hitimisho (Natumai, Nitashukuru…)
xi. Thibitisho: (Wako mwaminifu/mtiifu, sahihi, jina /cheo)
xii. Nakala kwa:

## 4. TAHARITI/BARUA YA GAZETINI ILIYOHARIRIWA

- ✓ mtajo (Mhariri,)
- ✓ Kichwa ()
- ✓ Utangulizi (Naandika kueleza…)
- ✓ Mwili (malalamiko, maoni, maombi, mapendekezo)
- ✓ Hitimisho (Natumai…)
- ✓ Thibitishio-jina na anwani ya mwandishi)

## 5. BARUA ZA MDAHILISI/PEPE

Barua ya aina hii hutumwa kwa tarakilishi kwa njia ya mtandao.

Jumatatu Novemba 30, 2007 saa 08:09:19
**Kutoka**: ishaj@gmail.com
**Kwa**: ahmed@african online.ke
**Nakala kwa**: amina @ mwananchi.com
**MINT/KUH**:
**Mwili**: Barua ya kawaida yenye maudhui kulingana na swali
**Hitimisho**: Aisha K Amira

## 6. MEME

Barua ambazo huhusisha matumizi ya ya vifaa vya umeme kama :
Tarakilishi
kiepesi/nukulishi/faksi
simu ya mkonono/tamba/rukono.

## 7. RISALA

Taarifa inayotoka kwa mtu au watu inayoeleza haja fulani k.m. risaala ya rambirambi, risala ya heri njema, ya waajiriwa kwa mwajiri au kinyume.
Kuna ya kawaida na rasmi. Ile rasmi huchukua muundo wa barua rasmi.

a). Rasmi
Muundo

i. Anwani ya mwandishi
ii. Tarehe
iii. Anwani ya m/warejelewa
iv. Mtajo
v. Kichwa: **RISALA YA RAMBIRAMBI……….**
vi. Ithibati kuwa umeiandika: Mimi wako…

## 8. MEMO

Martin Otunod Richard +254721246744

-Taarifa fupi ambayo huandikwa ofisini kuhusu mambo ya ndani kutoa maelekezo, maelezo au kukumbusha kuhusu jambo fulani. Ujumbe huwa mfupi na huhusu suala moja tu.

**SHULE YA UPILI YA GATWE**
**ANWANI:**
**MEMO**
**REJ:** km/01/06
**KUTOKA:** Mwalimu Mkuu
**KWA:** wafanyakazi wote
**MADA:** likizo fupi
**TAREHE:** 28/2/2011
**Ujumbe**:……..hapa ndipo maudhui huwa kutegemea swali
**SAHIHI**
**Jina**
**Cheo (mwalimu mkuu)**

**9. BARUA ZA MIALIKO**

Barua ambayo hupeleka taarifa kwa mtu kumuomba ahudhurie sherehe fulani.

**a) Rasmi (kadi au barua rasmi)**

**Muundo**

- ✓ Jina la mwalikaji/waalikaji (Bwana/mabwana/bibi/kasisi/daktari
- ✓ Jina la mwalikwa
- ✓ Sherehe (ndoa, mchango wa pesa, Kuna aina mbili za mialiko.
- ✓ Kusherehekea/kuadhimisha…)
- ✓ Kuhusu nani
- ✓ Mahali pa kukutanika
- ✓ Tarehe
- ✓ Wakati
- ✓ Anwani na nambari ya simu ya mwalikaji ambapo jibu litapelekwa kushoto chini (Majibu kwa…wima)

**b) Kirafiki (barua ya kirafiki)**

Sehemu ya mwili itoe habari zote muhimu katika mwaliko.

# B) INSHA NYINGINE

**10. RESIPE**

Jumla ya hatua na kanuni ambazo hufuatwa na mtu anapopika au kuandaa kitu mlo/kinywaji.

**Muundo**

**A). kichwa:**

- → unachoandika
- → chakula chenyewe
- → walengwa/idadi ya walaji
- → Hali yao….(kama ni wagonjwa taja ugonjwa wenyewe)
- → mfano : **RESIPE YA MAANDALIZI YA CHAI KWA WAGONJWA WANE WA KISUKARI**

**B). Viambata**

**-** Taja vitu vinavyohitajika pamoja na kiwango chenyewe

**C). Hatua za Upishi**

i. kila hatua ielezwe kwa utaratibu
ii. kila jambo lifuatwe

**D)** T*aja kitakacholiwa na ulichokipika bila kutaja upishi wake mf kitoweo(ulichoeleza upishi wake) kuandikwa mezani pamoja na ugali.*

**11. TAARIFA**

-Kuarifu kuhusu habari flani.
Kichwa:
Utangulizi:

Martin Otuno Richard +254721246744

Mwili:….**insha yenyewe kutegemea mahitaji ya swali**
Hitimisho:…..**namaliza kwa kusema kuwa……**
Ithibati:……**taarifa imeandikwa na (sahihi…………….jina……….)**

## 12. HOTUBA

-Maelezo yanayotolewa mbele ya watu.

✓ Hutolewa kwa usemi halisi na huanzia na kuishia kwa alama za usemi iwapo unamwandikia mwingine aisome kwa niaba yako lakini kama ni wewe mwenyewe usinukuu.

**Muundo**

A). **ANWANI**

i. **Hotuba**
ii. **Ya nani?**
iii. **kiini/kuhusu?**
iv. **Wapi?**

**Mf** **(HOTUBA YA MSHAURI KUHUS UMUHIMU WA USHAURI NASAHA KWA WANAFUNZI WA SHULE ZA UPILI KENYA)**

B). **UTANGULIZI** (kutaja hadhira kuanzia walio mashuhuri… kujitambulisha vyeo mabibi na mabwana na kuwakaribisha na kutambulisha kiini cha hotuba)

C). **MWILI**/Yaliyomo (kutaja na kufafanua hoja kulingana na mahitaji ya swali)

D). **HITIMISHO**

(shukrani na kuwatakia mema katika shughuli zao za kila siku/ AU kuwahimiza wafuate uliyowahutubia)

## 13. RATIBA

Mpangilio wa jinsi shughuli fulani inavyofanyika kulingana na wakati fulani uliotengwa k.m. sherehe ya arusi, mazishi, siku ya michezo, kutoa zawadi n.k.

**Muundo**

a. **Kichwa**
- → Ratiba ya shughuli gani?
- → ya nani?
- → Wapi?
- → Tarehe?

b. **Utangulizi**
- → Makaribisho
- → Maombi

c. **Mwili**
- → Shughuli yenyewe(mfano: harusi…)
- → Kutoa tuzo
- → Kutoa shukrani

d. **Hitimisho**
- → Kufungwa kwa maombi
- → Kuondoka/kufumkana

## 14. RIPOTI

Maelezo kuhusu mtu, kitu au tukio

a) **Ripoti ya Kawaida**

**Muundo**

- **Kichwa** (ripoti ya kamati/jopo gani)
- **Utangulizi** (maelezo mafupi ya jumla kuhusu mada husika)
- **Mwili**…insha itiririke kulingana na swali
- **Hitimisho** (matumaini, mwito kwa wengine wajiunge, wajitahidi)
- **Ithibati**: Ripoti imeandikwa na (jina, cheo/katibu, sahihi, tarehe)

b) **Ripoti rasmi/ Maalum**

**Muundo wake**

1. **KICHWA** (herufi kubwa na kupigiwa kistrari kirefu kimoja)

Martin Otunod Richard +254721246744

→ Unaandika nini?
→ ripoti ya jopo lipi?
→ Kuhusu/ kutathmini?
→ Wapi?

2. **UTANGULIZI/HADIDU ZA REJEA**
   i. Taja ripoti ilihitajika na nani?
   ii. uchunguzi ulifanywa kubainisha nini?
   iii. Nani wanajopo?

   Mfano: kutokano na ongezeko la wanafunzi kuacha shule kabala ya kuhitimisha masomo yao,waziri wa elimu bwa Matiangi alichagua jopo la kutathmini na kupendekeza suluhu ya janga hili sugu kwani kilicho na mwanzo lazima kina mwisho, miongoni mwa wanajopo hao ni:
   a. ………Mwenyekiti
   b. ………Katibu
   c. ……….Mwekahazina
   d. ……….mwanachama

3. **UTARATIBU/MBINU/ HATUA ZA UTAFITI**

   Wanakamati walihusisha mbinu zifuatazo ili kupata habari za kutegemea
   i. Kuhoji…
   ii. hojaji ……,
   iii. ilipiga picha za video
   iv. mashauriano

4. **MATOKEO**

   Kamati iligundua kuwa :
   a) ………………
   b) ………………
   c) ………………..
   d) ………………
   e) ……………..
   f) ………………..

5. **MAPENDEKEZO** (suluhisho la shida)

   Ili kupambana na janga hili sugu, kamati/jopo lilipendekeza hatua zifuatazo kufuatwa:
   a) ………………
   b) ………………
   c) …………………
   d) …………………
   e) …………………
   f) ……………

6. **HITIMISHO**

   **Andika maandishi yanayonuia kuelekea/kuegemea kuwa iwapo mapendekezo yaliyotolewa yatafuatwa basi janga hili litazikwa katika kaburi la sahau**

7. **ITHIBATI**

Ripoti imeandikwa na:
Katibu…………………………………………………sahihi…………………tarehe…………………………………

## 15. DAYALOJIA/MAZUNGUMZO

Mazungumzo kati ya watu wawili au zaidi kuhusu jambo au mada fulani

**Muundo**

**a. Kichwa**

Kichwa kizuri kitaje:
i). Ni dayalojia ya nani na nani?
ii). Kuhusu nini?
iii). Wapi?(ingawa si lazima)
mfano
DAYALOJIA BAINA YA WAZIRI WA USALAMA NA MWANAHARAKATI (BW. KALINDE) AFISINI MWAKE

Martin Otunod Richard +254721246744

**b. Utangulizi**

i). mwanafunzi awafanye wahusika wake kuamkuana
ii). Mmoja(mwenyeji) amkaribishe mwenzake
iii). Watangulize mada/sababu ya dayalijia yao

**c. mwili**

i). Hoja zote zijumuishwe kwenye dayalojia

**d. hitimisho**

i). Hitimisho idhihirike aidha kwa muhtasari wa waliyokuwa wakizungumzia au
ii). Shukrani na kuagana

## 16. MAHOJIANO

Mazungumzo yanayoendeshwa kwa muundo wa maswali na majibu(kudadisidadisi)

**Muundo**

**a. Kichwa**

Kichwa kizuri kitaje:
i). Ni Mahijianokati ya nani na nani?
ii). Kuhusu nini?
iii). Wapi?(ingawa si lazima)
mfano
<u>MAHOJIANO BAINA YA WAZIRI WA USALAMA NA MWANAHARAKATI(BW. KALINDE) AFISINI MWAKE</u>

**b. Utangulizi**

i). mwanafunzi awafanye wahusika wake kuamkuana
ii). Mmoja(mwenyeji) amkaribishe mwenzake
iii). Watangulize mada/sababu ya dayalijia yao

**c. mwili**

i). Hoja zote zijumuishwe kwenye dayalojia huku wahusika wote wakishirikishwa vilivyo na kuonyesha umahiri wao wa mada.

**d. Hitimisho**

i). Hitimisho idhihirike ; aidha kwa muhtasari wa waliyokuwa wakizungumzia au
ii). Shukrani na kuagana

## 17. KUMBUKUMBU

Maelezo kuhusu yaliyojadiliwa na kuafikiwa katika mkutano.

**Muundo**

- Kichwa
  Mfano: **KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA KAMATI/JOPO GANI, ULIOFANYIKA WAPI, TAREHE GANI, SAA NGAPI HADI GANI NA MAJIRA**
- **Waliohudhuria** (mwenyekiti, katibu, mweka hazina, wanakamati)
- **Waliotuma udhuru** kwa kutohudhuria
- **Waliokosa** kutuma udhuru wa kutohudhuria
- **Waalikwa-**(si lazima iwepo)
- **Ajenda**

a) **Kufunguliwa** kwa mkutano (KUMB 3/2009)
✓ Kufunguliwa kwa mkutano, mwenyekiti kuwakaribisha na kuwashukuru waliohudhuruia na kumwomba … aongoze kwa maombi.
b) **Kusoma na kudhibitisha** kumbukumbu za mkutano uliotangulia
✓ Kusomwa na katibu, aliyependekeza na aliyedhibitisha.
c) **Masuala yaliyotokana** na kumbukumbu hizo
✓ (a) KUMB 8/2008 ununuzi wa miti
**d) Shughuli nyinginezo**
e) **Kufunga mkutano** (KUMB 7/2009)
✓ Mkutano uliisha saa ngapi?
✓ maombi yaliongozwa na nani?
✓ mukutano mwingine ukapangwa kuwa siku gani?

Martin Otunod Richard +254721246744

- Maneo kama walikubaliana, waliafikiana, alipendekezwa, ilisemekana, waliambiwa, ilionelewa ni bora, walishauriwa, ilidaiwa, aliomba, n.k.

**THIBITISHO**
KATIBU TAREHE…………… SAHIHI ……………
MWENYEKITI TAREHE …………... SAHIHI ……………

**18.** **SHAJARA**

Daftari ambayo huhifadhiwa matukio yanayofanyika kila siku.

**Aina**

**a) Ya kibinafsi**

Huwa na:

i. Siku
ii. Tarehe
iii. mwaka

JUMANNE 30/8/2016

iv. Tukio lililohudhuriwa/tokea

Mfano

**JUMATANO/01/12/16**

Nilimtembelea Mwalimu wa Kiswahili kule Lenga Juu na tukaenda naye kwenye maktaba ya serikali kutafiti kuhusu changamoto za lugha ya Kiswahili

ALHAMISI 02/12/2016

Nilifanya kazi zangu na kuwatembelea waathiriwa wa mkasa wa shambulizi la kigaidi wa Waste Gate.

**b) Rasmi (hutumiwa katika ofisi)**

Hutumika afisini

**19.** **TAHADHARI/ ONYO**

Makatazo/Julisho kuhusu jambo la hatari.

**Muundo**

i. **Anwani** : JITAHADHARI NA WIZI WA MTIHANI
ii. **Utangulizi:…**Kutokana na……./Ningependa kuwatahadharisha dhidi ya….
iii. **Mwili**: hapa ndipo hija/maudhui hujadiliwa kwa kina
iv. **Hitimisho**……………..toa msimamo
v. **Ithibati/mwandishi/anayeonya**

**20.** **ILANI /NOTISI**

Julisho, tangazo au notisi.

**Muundo**

a) Tarehe ……………………..
b) Kutoka:
c) Kwa:
d) Rej:……OBM/001
e) **Anwani** : KUKIUKA SHERIA KAZINI
f) **Utangulizi:…**Kutokana na……./habari zinazonifikia afisini mwangu….
g) Mwili: hapa ndipo hija/maudhui hujadiliwa kwa kina
h) Hitimisho……………..toa msimamo

**21.** **TAHAKIKI**

Maandishi ya kuchambua maandishi ya fasihi.

Mfano wa mambo yanayoweza kuhakikiwa na mtahiniwa tahakiki Kukirejelea Riwaya ya K. Walibora ya *Kidagaa kimemwozea*

**KIDAGAA CHAWAOZEA WANAJAMII**

**1. Sura**

**Anwani**: Kidagaa kimemwozea
**Mwandishi:** K. Walibora
**Mchapishaji:** Oxford University Press

Martin Otunod Richard +254721246744

**Mhakiki**: A. G Rugiha
**Bei :** shilingi 450 za Kenya
**Mada:** TAHAKIKI YA RIWAYA YA KIDAGAA KIMEMWOZEA

2. **Maudhui**

Baadhi ya maudhui yanayoweza kuhakikiwa na mwanafunzi ni pamoja na:

i. Anwani
ii. dhamira
iii. maudhui
iv. wahusika
v. uhusika
vi. mandhari
vii. mbinu za kisanaa
viii. tamathali za usemi
ix. usasa/ukale wa kazi
x. Jalada. n.k

**TANBIHI:**Hapa mwanafunzi anahitaji kujadili iwapo vipengele hivi viliafikiwa na mwandishi wa kitabu au la!

## 22. MATANGAZO

Haya ni Majulisho kuhusu jambo fulani.

**a) Arifa**

SHULE YA UPILI YA MWANGAZA
Anwani, tarehe
USAJILI WA …
Sahihi
Jina
Cheo

**b) Kibiashara**

**Sifa**

- ✓ Chuku
- ✓ Lugha nyepesi
- ✓ Takriri
- ✓ Alama ya (!) na (?)
- ✓ Michoro
- ✓ Maonyo
- ✓ Maelezo kukihusu
- ✓ Kinavyotumika
- ✓ Ubora wake
- ✓ Watengenezaji

**c). Kifo**

TANGAZO LA KIFO
Tunasikitika kutangaza kifo cha …Alikuwa…
Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi

**d). kazi**

NEMBO SHULE YA UPILI YA MWNGAZA
ANWANI :NAFASI YA KAZI YA UHASIBU
TAREHE:01/12/2016
sifa za mwomba kazi

**JINSIA**

Awe wa jinsia ya kiume.

**UMRI**

Awe na umri wa miaka isiyopungua23 na isiyozidi 32.

**ELIMU**

i. Awe na shahada ya uhasibu kutoka chuo kikuu kinachojulikana au awe na shahada ya diploma ya juu ya uhasibu

Martin Otunod Richard +254721246744

ii. Awe amepata alama ya c katika kingereza

**KAZI**

i. Kuidhinisha hati za malipo za shirika

ii. Kusimamia shughuli za uhasibu katika idara inayohusika

**UZOEVU/TAJRIBA**

Awe na uzoevu wa kazi usiopungua miaka 5 kwenye shirika au taasisi kubwa.

**DINI**

Awe muumini wa dini ya kikristu na awe ameokoka.

**MUDA WA KAZI**

Kuanzia saa mbili hadi saa kumi na moja jioni na masaa mengine ikibidi.

**MSHAHARA**

Mshahara utategemea elimu ya anayehusika lakini utakuwa baina ya ksh 24,000 na ksh 45000.

**MAELEZO YA ZIADA**

Maombi yote yawe yamewasilishwa kabla ya tarehe 30 mei 2010.

Maombi yatumwe kwa:

**Katibu,**

**Halmashauri ya shule ya upili ya Mwangaza ,**

**Anwani:**

Maombi yatakayopelekwa baada ya muda wa mwisho hayatajibiwa.

Maombi yaandamane na hundi ya shilingi elfu moja ambazo hazitarejeshwa.

**23.** WASIFU

Maelezo ya mtu yakitolewa na mtu mwingine tangu kuzaliwa mpaka alipo au kufa kwake.

**muundo**

- ✓ **anwani**
- ✓ **kuzaliwa**
- ✓ **mahali**
- ✓ **masomo**
- ✓ **mafanikio na udhaifu wake**
- ✓ **hitimisho**

**mfano wa anwani:**

**WASUFU WA MWALIMU WANGU BW. RUGIHA**

**24.** TAWASIFU

Maelezo ya mtu kujihusu

**ANWANI: TAWASIFU YANGU(BW. AKARANGA)**

**Vidokezo**

i. Jina lake/lako
ii. Jinsia.
iii. Eneo unakotoka.
iv. Umri.
v. Kuzaliwa.
vi. Maumbile/mme/mke
vii. Elimu- Kuanzia kwa ya hivi karibuni hadi ya kwanza
viii. Kazi
ix. Hadhi ya ndoa
x. Lugha
xi. Lakabu na sababu
xii. Umaarufu
xiii. Uraibu.
xiv. Warejelewa/wahisani

**25.** WASIFUTAALA/WASIFU KAZI

Maelezo rasmi kuhusu mtu binafsi ambayo huambatanishwa na barua ya kuomba kazi.

**WASIFUTAALA WANGU**

Martin Otunod Richard +254721246744

**1. MAELEZO BINAFSI**

**Jina** : Frenkel Akaranga Rugiha
**Tarehe ya Kuzaliwa** : 31/12/1988
**Umri** : miaka 27
**Mahali pa kuzaliwa** : Voi
**Jinsia** : mwanamke
**Hadhi ya ndoa** : Nimeolewa/kapera
**Nambari ya kitambulisho** : 12345678
**Uraia** : Mkenya
**Lugha** : Kiswahili, Kingereza, Kikuyu
**Anwani ya kudumu** : S.L.P. 1600, Voi
**Barua pepe** : Frenkelakarugi@yahoo.com
**Simu tamba** : 0726044433

**2. ELIMU:**

**2010-2014**: Chuo Kikuu cha Masinde Muliro –shahada ya ualimu (Kiwango cha pili cha juu)
**2004-2007**: Shule ya upili ya Shimoni (Shahada ya KCSE)
**1995-2003**: Shule ya Msingi ya Umazi (shahada ya KCPE)

**3. TAJRIBA**

**2015-Mpaka sasa**: Mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya upili ya Tung'are
**2013-2015:** Mwalimu wa Kiswahili shule ya upili ya ushindi.

**3. HABARI ZA ZIADA**

**URAIBU**

a) Kusoma vitabu vya sarufi na fasihi
b) Kutembelea wajane, mayatima na wagonjwa
c) Kuandika mashairi

**4. AZIMIO LANGU**

a) Kupaa kitaaluma kwa kuendeleza masomo yangu hadi kiwango cha uzamifu
b) Kuwa mhasibu bora zaidi nchini kwa matendo na kuwapa wananchi huduma za kufaa

**5. WAREJELEWA**

1. **Profesa simala inyani ,**
   **Chuo Kikuu masinde muliro**
   **S.L.P.43844,**
   **Mwanzo.**
2. **Maimuna Njavu Mukota,**
   **Shule ya Upili ya Alliance,**
   **S.L.P. 6744,**
   **Nairobi.**

Martin Otunod Richard +254721246744

**26. MAAGIZO/MAELEKEZO**

✓ Maelezo kuhusu namna ya kufika mahali kutoka kituo fulani au maelezo kuhusu njia ya kutumia kitu au huduma fulani.

**Sifa**

a) Maelezo wazi
b) Michoro au ramani
c) Dira
d) Huhusika maonyo
e) Tarakimu k.m. 1×3
f) Matumizi ya herufi nzito.

**Mifano**

a) Maagizo ya daktari kwa mgonjwa wa kisukari.

b) Maelekezo ya kutoka nyumbani hadi shuleni mwenu.
c) Jinsi ya kutumia dawa za wadudu

**27. KUJAZA FOMU**

Fomu ni Karatasi ambayo ina nafasi ya kuandika maelezo ambayo yanatakiwa.
Maelekezo ya jinsi kuikabili insha hii:

a) Soma fomu kwa makini kabla ya kujaza chochote.
b) Andika maelezo kwa muhtasari.
c) Usijaze kama huna hakika kwenye sehemu Fulani.
d) Usifutafute.
e) Itumie alama inayostahili wakati wa kujaza fomu.

**muundo**

**1. MAELEZO YA KIBINAFSI**

**TAREHE**……………………………………………….
**JINA**…………………………………………………………
**JINSIA**……………………………………………………………
**UMRI**……………………………………………………
**TAREHE YA KUZALIWA**……………………………………
**URAIA**…………………………………………….
**NAMBARI YA KITAMBULISHO**……………………………
**KAZI**…………………………………………………
**MKOA**……………………………………………………………
**WILAYA**……………………………………………………
**SIMU**…………………………………………………………
**SAHIHI**…………………………………………………
**TAREHE**…………………………………………………..

**28. HOJAJI**

Maswali ambayo hutumiwa kama msingi wa kufanyia utafiti na huelekezwa kwa mhojiwa.

**Aina**

**i. Hojaji Wazi**

Hojaji yenye maswali ambayo mhojiwa anaruhusiwa kuyajibu kwa maneno yake mwenyewe.

**UCHAGUZI NA VIONGOZI**

1. Una maoni gani kuhusu uchaguzi wa kila baada ya miaka mitatu?
…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
2. Kwa nini una maoni hayo?
…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
3. Wewe ungependelea utaratibu gani wa uchaguzi?
…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
4. Je ni kweli viongozi hung'ang'ania mamlaka?
…………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………
5. Je viongozi hung'ang'ania uongozi kwa sababu zipi?

a) ………………………………………………………………………………………………………………
b) ………………………………………………………………………………………………………………
c) ………………………………………………………………………………………………………………

**ii. Hojaji Funge**

✓ Hojaji ambapo mhojiwa anapewa majibu kadha ambayo anatakiwa kuchagua mojawapo bila kuwa na uhuru wa kuandika atakayo.

**MATATIZO YA KIJAMII**

Martin Otundo Richard +254721246744

Tia alama kwenye jibu unaloafiki

a) Jamii yetu inawakandamiza wanawake?
Ndiyo (   )  La (   )

b) Tatizo kubwa la jamii yetu kwa sasa ni umaskini na ugonjwa.
Kweli (   )  Si kweli (   )

## 2. INSHA ZA KUJADILI

Kwa sasa huja kama swali la pili katika mtihani wa kitaifa KCSE
Baadhi ya maneno yenye utata:

- **Kujadili**-mwanafunzi yafaa aeleze hoja kwa undani

Swali linaweza kujadiliwa upande mmoja au kuwili kutegemea mahitaji ya swali

- **Fafanua/thibitisha/eleza**

Hapa mwanafunzi yampasa aandike kulingana na wazo/kauli ya mtahini.

- **Kuliko/kushinda**- mtahini ajadili hoja nyingi upande mmoja ikilinganishwa na upande mwingine.
- **.....'ni kama sarafu'**-swali lishughulikiwe kuwili

## 3. INSHA YA METHALI

i. Mwanafunzi asimulie kisa cha kuvutia kutegemea maana ya ndani ya methali
ii. Asitoe maana ya methali
iii. Pande mbili zijitokeze bayana (sivyo itakuwa imelemaa na atasahihishwa chini ya 10 C+)
iv. Lazima pande hizo mbili zikamilike(asiandike upande mmoja na kutua kwingine gafla)

## 4. KUANZISHA DONDOO/(KUMALIZA KWA MANENO ALIYOPEWA)

(i) Mtahiniwa anatarajiwa kubuni kisa kizuri ili:
(ii) Amalizie/Kutanguliza kwa maneno hayo. Anayekosa kumalizia/kuanzia kwayo amejitungia s wali atuzwe **D 02/20 au 03/20**
(iii) Anayeongeza maneno chini ya matano, achukuliwe kuwa na kosa la mtindo na akadiriwe ifaav yo.
(iv) Anayekata au kusahau meneno chini ya maneno achukuliwe kuwa nakosa la kimtindo;akadiri we ifaavyo.
(v) Kisha cha mtahiniwa sharti kionyeshe mhusika aliyepitia hali inayoelekezwa na maneno hayo.

**Uhusika**
Asiyezingatia nafsi iliyo kwenye dondoo atuzwe D 02/20 au 03/20.

# MWONGOZO WA KUDUMU WA KUSAHIHISHA INSHA TANGU 2012 HADI SASA

Karatasi hii imeandikwa kutahini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi. Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtanhiniwa, kwa mfano,

- Kutunga sentensi sahihi, zenye utiriko mizuri kimawazo, lugha ya kuvutia na yenye mawazo asilia,
- Ubunifu mwingi
- Hati nadhilfu.
- Kutegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha.
- Lazima mtahini atilie maanani mtindo, mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagaizo vilivyo.
- Viwango mbalimbali vilivyopendekezwa ni : **A**, **B**, **C**, ama **D** kutegemea mahali popote pale pafaapo kama ifuatavyo:

**VIWANGO TOFAUTI VYA D (01-05)**
**D- (01 – 02):**
1. Insha hii haina mpangilio maalumu na haieleweki

Martin Otuno Richard +254721246744

2. Mtahiniwa anaweza kunakili swali au akajitungia swali na kujibu.
3. Anaweza kuankili kichwa na kasha kuishughulikia.
4. Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili

**D (03):**
1. Utiririko wa mawazo haupo.
2. Insha haieleweki.
3. Makosa ni mengi sana.
4. Mtahiniwa anapotoka kimaudhui(kutoelewa swali)
5. Hakuzingatia urefu.

**D+ (04 – 05):**
1. Mtahiniwa ana lugha dhaifu ya Kiswahili na haina mpangilio.
2. Ana makosa mengi ya kila aina.
3. Mtahiniwa anaweza kutambua kila mtahiniwa anajaribi kuwasilisha.
4. Mpangilio wa kazi ni hafifu mtahiniwa hujirudia.
5. Mtahiniwa ana athari za lugha ya kwanza kwa mfano papa badala ya baba

**KIWANGO CHA C (MAKI 06 – 10):**

**Kiwango hiki kina makosa yafuatayo**
1. Mada haikukuwa na kuendelezwa
2. Anawasilisha ujumbe kwa njia isiyovutia.
3. Hana ubunifu wa kutosha.
4. Anaakifisha sentensi vibaya.
5. Hana msamiati wa kuvutia wala msamiati mwafaka.
6. Kuna makosa ya hijai, sarufi na msamiati.

**VIWANGO TOFAUTI VYA C**

**C- (06 – 07):**
1. Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha mawazo yake.
2. Hana msamiati ufaao wala muundo wa sentensi ufaao.
3. Ana makosa mengi ya sarufi hijai na msamiati.
4. Mada haikukuwa wala kuendelezwa kwa njia ifaayo.
5. Matumizi ya tamathali ya usemi yanadhihirika.
6. Makosa ya sarufi ni hijai ni machache.
7. Sarufi yake ni nzuri.

**C (WASTANI- 08):**
1. Anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu.
2. Hana ubunifu wa kutosha na dhana tofauti hazijitokezi wazi.
3. Uakifishaji wa sentensi zake si mzuri.
4. Amejaribu kushughulikia mada aliyopewa.
5. Ana makosa ya hijai sarufi na msamiati

**C+ (09 – 10):**
1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri lakini kwa njia isiyo na mvuto.
2. Dhana tofauti tofauti zimeanza kujitokeza japo kwa njia hafifu
3. Kuna mtiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa.
4. Misemo, methali na tanakali za sauti zimetumiwa kwa njia hafifu.
5. Amashughulikia mada alivyopewa kwa utiririko mzuri.
6. Kuna makosa ya sarufi msamiati na hijai lakini bado inaeleweka.

**KIWANGO CHA B (MAK) 11- 15)**
1. Katika kiwango hiki mtahiniwa anaonyesha kuimudu lugha vilivyo.
2. Mtaniniwa anadhihirisha kwamba anaweza kutumia lugha kwa urahisi katika kujieleza.

Martin Otunod Richard +254721246744

3. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri.
4. Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha kama vile kuandika sentensi kwa njia tofauti tofauti na zikaleta maana sawa sawa.
5. Mada inakuzwa na kuendelezwa kikamilifu.

**VIWANGO TOFAUTI VYA B**

**B- ( 11 – 12):**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe wake kwa kuonyesha hoja tofauti.
2. Kuna utiririko mzuri wa mawazo.
3. Anauwezo wa kutumia miundo tofauti tofauti ya sentensi.
4. Makosa ni michache ya hapa na pale.

**B (WASTANI) (MAK 13):**

1. Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kumudu lugha.
2. Anawasilisha ujumbe wake waziwazi kwa mawazo yayodhihirika..
3. Matumizi ya lugha ya mnato yamejitokeza.
4. Anatumia mifano michache ya msamiati mwafaka.
5. Matumizi ya tamathali za semi yanaanza kudhihirika.
6. Makosa yanaweza kutokea hapa na pale.

**<u>B+ (14 – 15)</u>:**

1. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika.
2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe wake kwa njia inayovutia kwa urahisi akizingatia mada.
3. Kuna makosa ya hapa na pale ambayo mtahiniwa hakughamiria.
4. Uteuzi wake wa msamiati ni mzuri.
5. Sarufi yake ni nzuri inayovutia na kwa urahisi akizingatia mada.
6. Uakifishaji wake ni mzuri.
7. Makosa hutokea hapa na pale.

**KIWANGO CHA A (MAKI 16-20)**

1. Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi kwa lugha yenye mnato. Ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka.
2. Ana uwezo wa kutumia tamadhali za lugha ili kutoa hisia zake kwa njia bora na kwa urahisi.
3. Umbuji wake hudhihirisha ukakamavu wake kimawazo na mpangilio mzuri na hali ya kumvutia masomaji wake.
4. Kazi ya mtahiniwa ni nadhifu na hati ni nzuri.
5. Insha hii imezingatia urefu unaotakikana.
6. Insha yoyote ile ya kiwango cha A, sharti awe urefu wa maneno 400.

**VIWANGO TOFAUTI VYA A**

**A- (16 – 17):**

1. Mtahiniwa hudhihirisha ukomavu wa lugha.
2. Ana utiririko mzuri wa mawazo kulingana na mada.
3. Huipamba lugha yake kwa kutumia tamathali za usemi.
4. Huzingatia matumizi mazuri ya msamiati na sarufi.
5. Makosa ya kawaida ya lugha ni nadra sana kupatikana makosa machache yasiyokusudiwa hutokea.

**<u>A (MAKI 18)</u>:**

1. Mawazo yanadhihirika zaidi na anashughulikia mada aliyopewa
2. Makosa ni machache mno.
3. Hutumia lugha ya mnato.
4. Hutumia msamiati wa hali juu.
4. Sarufi yake ni nzuri.
6. Hutumia miundo tofauti ya sentensi kifundi
7. Hujieleza kikamilifu na makosa ni nadra kupatikana.

**A+ (19 – 20):**

Martin Otunod Richard +254721246744

1. Mtahiniwa huwasilisha ujumbe kulingana na mada.
2. Hudhihirisha mawazo yake vizuri.
3. Hujieleza kikamilifu bila shida na kwa urahisi.
4. Ametumia njia zilizokomaa.
5. Makosa yoyote yale yasipite matano.
6. Msamiati wake ni wa hali ya juu sana.

## BAADHI YA MASUALA IBUKA ANAYOWEZA KUTARAJIA MTAHINIWA

**1. JINSI YA KUJIKINGA NA MAGONJWA**

i. Kula chakula chenye virutubisho vyote na madini
ii. Kutotumia chumvi, sukari au mafuta mengi
iii. Kufanya mazoezi
iv. Kupimwa mara kwa mara
v. Kupika vyakula vizuri
vi. Kunawa mikono na macho
vii. Kuchemsha maji au kuyatia dawa kabla ya kuyanywa
viii. Kutozini au kutumia kinga
ix. Chanjo kwa watoto
x. Kutochangia vifaa kama vitana na nyembe na mavazi ili kujikinga na magonjwa ya ngozi.
xi. Kulala ndani ya neti iliyotiwa dawa
xii. Kufyeka nyasi karibu na nyumba na kutupa mikebe iliyo na maji
xiii. Kuweka dawa kwenye vidimbwi ili kuua mbu
xiv. Kutotumia vileo kama vile pombe na sigara
xv. Kuzuia kunyeshewa na mvua na kuvaa mavazi mazito wakati wa baridi au usiku
xvi. Kukohoa au kupiga chafya mtu akiwa ameziba pua na midomo
xvii. kutotema kikohozi ovyo.
xviii. Kutubu dhambi, kujua Mungu na kuomba kwa afya ya kiroho.

**2. UNYANYASAJI/UDUNISHAJI WA WAN AWAKE NA UTAMADUNI/TAASUBI Z A KIUME**

**a). Namna/njia za unyanyasaji**

i. Kutorithi mali
ii. Wanawake wajane kunyang'anywa mali na k ufukuzwa
iii. Ndoa za wake wengi (uke wenza).
iv. Kurithi wanawake (wajane) kwa lazima.
v. Kukeketwa.
vi. Kutawishwa au kunyimwa uhuru wa kutoka
vii. Kutoelimishwa eti kwa akiolewa hatafaidi fa milia, atapanda wanaume vichwa au atakuw a malaya
viii. Ndoa za mapema/lazima zinazosababisha ku katiza elimu yake (mahari haiwezi kurudish wa).
ix. Kulazimishwa kuolewa na mtu asiyempenda .
x. Kunyimwa haki ya kusema.
xi. Kupigwa na kutusiwa
xii. Kubakwa.
xiii. Kunyimwa ajira kwa vile akipata mimba ataj ikokota kazini na atahitaji likizo baada ya ku jifungua.
xiv. Ajira ya mtoto wa kike ambapo anafanyishw a kazi ya sulubu na kupewa mshahara duni
xv. Kutalikiwa.
xvi. Wanaume kutokuwa waminifu kwao hata ku wanyima mahitaji na kuwapa mahawara zao
xvii. Wanaume kupuuza majukumu ya kukimu fa milia.
xviii. Ubadhirifu wa wanaume na hali wake zao n dio walifanya kazi za kupatia hizo pesa
xix. Kulaumiwa mtoto akikosekana hata mke m wingine kuolewa
xx. Mahali pa mwanamke kuwa nyumbani au ha ruhusiwi kufanya kazi ofisini au kuongoza
xxi. Kulazimishwa kuvaa mavazi aina fulani na k ukatazwa kuvaa aina mengine
xxii. Kufanyishwa kazi za nyumbani kama mtum wa.
xxiii. Kudhibitiwa na wanaume zao kwa sababu y a wivu.

**b). Suluhisho**

a) Hatua kali za kisheria kwa wanaowapiga, w anaowabaka na wanaotekeleza mila ya kuke keta na ndoa za mapema
b) Kufanya kampeni dhidi ya mila zinazochang ia udunishaji wa wanawake
c) Kuwashauri watoto wa kike badala ya kuwa pasha tohara waende shuleni
d) Kuanzisha makao ya watoto wa kike wanaot ishiwa na mila mbaya
e) Kumwelimisha mwanamke kuhusu haki zak

Martin Otundo Richard +254721246744

e

f) Kuhimiza wanawake kupigania haki zao

g) Serikali kutenga pesa za kuelimisha watoto wa kike ili kuwapa uwezo wa kiuchumi kwa ni wengi hunyanyaswa kutokana na umaskin i na ujinga.

h) Mashirika ya kutetea haki za wanawake kam a FIDA na Maendeleo ya Wanawake.

i) Hazina ya kutoa mikopo kwa makundi ya w anawake k.v. K.W.F.T

j) Kuwapa wanawake nafasi sawa za ajira

k) Kutekelezwa kipengele cha thuluthi ya wana wake katika uongozi.

l) Kupunguza alama ambazo wasichana wanaz opaswa kufikisha ili kujiunga na vyuo vya el imu ya juu.

m) Kubuni sheria za kuwawezesha kumiliki mal i

### 3. JINSI WANAUME/VIJANA WA KIUME WANAVYODHULUMIWA

i. Kupigwa na wazazi/waelekezi wao

ii. Kuchomwa kwa maji moto

iii. Kukatwa sehemu nyeti

iv. Wanawake kutokuwa waminifu kwao.

v. Kutusiwa

vi. Kutofuliwa nguo na wake zao.

vii. Kunyimwa chakula.

viii. Kutelekezwa.

ix. Kunyimwa unyumba kama njia ya kulipiza k isasi au kumwadhibu

x. Kazi za sulubu.

xi. Kufanyishwa kazi fulani k.v. kufulishwa ngu o na kupikishwa mke akiwepo hata mbele ya wageni

xii. Kuzomewa/ kugombezwa wake.

xiii. Kunyimwa pesa kama hana ajira.

**b). suluhu**

- Hatua kali za kisheria k.m kufunwa jela kwa wanaowapiga na kuwatelekeza.
- Kufanya kampeni dhidi ya mila zinazochang ia udunishaji wa waume.
- Kuwashauri watoto wa kiume dhidi ya kuwa kabili wake bila uhasama.
- Kumwelimisha mwanamme kuhusu haki zak e.
- Serikali kutenga pesa za kuelimisha vijana w a kiume ili kuwapa uwezo wa kiuchumi kwa ni wengi hunyanyaswa kutokana na umaskin i na ujinga.
- Mashirika ya kutetea haki za waumme yaun dwe.
- Kuwapa wanaume nafasi sawa za ajira.
- Kusawazisha alama za wanafunzi kujiunga n a vyuo vya elimu ya juu.

### 4. UFISADI

Uovu, ubaya au uharibifu.

**a). Aina shuleni**

i. Wanafunzi kudanganya katika mtihani

ii. Kutoza mwanafunzi wa kidato cha kwanza p esa au chakula kama nyama ili kuwalinda.

iii. Kujipakulia chakula kingi.

iv. Waalimu wakuu kuitisha hongo ili kuruhusu wanafunzi wajiunge na shule zao

v. Kupita wengine katika foleni wanapokwend a kupata chakula au chai hata benki

vi. Kurudishiwa bakaa/chenji nyingi dukani na kutoirejesha kwa muuza duka.

vii. Kuokota pesa njiani na kutoulizia ni za nani

viii. Kughushi stakabadhi za mtihani, hati za umi liki shamba.

ix. Kunakili kanda za muziki za wengine na kuz iuza.

x. Waajiri kuajiri watu wa familia zao au maka bila yao.

xi. Daktari kuitisha hongo ili amhudumie mgon jwa

xii. Polisi kuitisha hongo ili aruhusu magari ya h uduma kwa umma yasiyofaa kupita

xiii. Kutohoa maziwa au kuyaongezea maji ili ya we mengi

xiv. Wenye maduka kuuza bidhaa kwa bei ghali

xv. Kuuza bidhaa kama sukari, nyama, nafaka, g esi na mafuta ya petroli ambazo hazijatimiza uzani unaotakikana

xvi. Madereva wanaoendea mafuta ya petroli ku uza kiwango fulani cha hayo mafuta na kuon gezea ya taa au diseli

xvii. Kuuzia watu dawa bandia zisizotibu magonj wa

xviii. Ulanguzi wa dawa za kulevya

xix. Kuiba pesa kwa kutumia risiti bandia au kuf uruisha bei za bidhaa ili pesa zilizo juu wahu sika wagawane

xx. Kutoa ushahidi wa uongo

xxi. Kunyang'anya wajane na yatima mali zao

xxii. Uporaji wa mali ya umma k.v. nyanja za kuc hezea watoto na misitu

xxiii. Hakimu kuchukua hongo aididimize kesi

xxiv. Madaktari kutoza wawele ada ya juu hata ku wafanyia upassuaji wasiouhitaji ili wapate p esa.

xxv. Wafanyakazi wa halmashauri za miji kujific ha wanapomwona mtu akiegesha gari ili wa dai anakwepa kulipa ada ya uegeshaji ili wa hongwe au walikokote gari wapate pesa zaid i.

**b). Sababu Ya Watu Kuushiriki Ufisadi**

a) Tamaa ya kutajirika

b) Kutofahamu madhara/matokeo yake

c) Kukosa njia za kukimu mahitaji

d) Mishahara au mapato duni yasiyomwezesha mtu kukimu mahitaji yake au ya familia

e) Kutotosheka kwa kile mtu alichonacho.

f) Hofu ya kupata hasara au kukosa ajira.

g) Kutomjua mungu hivyo hawana imani.

Martin Otundo Richard +254721246744

h) Kuzugwa au kutekwa nyara kimawazo na kuwa mtumwa na shetani.
i) Wengine hulichukulia kama jambo la kawaida tu au hali ya maisha.
j) Imani kuwa siku hizi mtu hawezi kupata chochote bila kutoa hongo.

**c). Madhara ya ufisadi**

i. Vifo kutokana na aajali barabarani au kutotibiwa bila hongo.
ii. Majeruhi wa ajali za ajalini wengine hulemaa wasiweze kujifanyia kazi zao.
iii. Kufutiliwa kwa matokeo ya mtihani .
iv. Kufukuzwa shuleni au chuoni.
v. Umaskini kutokana na utoaji hongo ya pesa nyingi kisha kutopata kazi na ununuzi wa bidhaa kwa bei ghali.
vi. Kushuka kwa viwango vya elimu wasiohitimu ipasavyo wanaporuhusiwa kujiunga na shule/ vyuo fulani
vii. Kushuka kwa viwango vya huduma kwa umma kutokana na kuajiriwa kwa watu wasiohitimu vizuri.
viii. Afisi za serikali kuchomwa wafisadi wakijaribu kusitiri ushahidi wa ufisadi
